

## COUNTY GOVERNMENT OF LAMU



## THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU

### THE HANSARD

Tuesday, 9<sup>th</sup> December, 2025

*The Assembly met at the  
Main Chambers, at 2:30 p.m.*

[Deputy Speaker (MCA Paul Kimani Njuguna) in the Chair]

### PRAYERS

**Deputy Speaker** (MCA Paul Kimani Njuguna): Next Order.

**Clerk-at-the-Table:** Notices of Motion

### NOTICES OF MOTION

#### *PROTECTION AND COMPLETION OF STALLED AND PREVIOUSLY INITIATED PROJECTS IN LAMU COUNTY*

**MCA Fahd Dini Adnan** (*Nominated*): Thank you Mr Deputy Speaker. Mr Deputy Speaker Sir, I beg to give the following Notice of Motion: -

**AWARE THAT**, article 201 of the Constitution of Kenya requires that public finances be managed in a prudent and responsible manner, ensuring accountability and safeguarding public resources from wastage.

---

*Disclaimer: The electronic version of the Assembly Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Office of the Clerk.*

**FURTHER AWARE THAT**, Section 30(3)(f) of the County Governments Act mandates the County Executive to ensure effective service delivery, while Sections 104 and 105 of the Public Finance Management Act direct County governments to ensure efficient, economical and transparent use of public funds.

**CONCERNED THAT**, in Lamu County several key development projects initiated under previous regimes including the Mai Mekoni Water Project, the Myabogi footbridge and the Mtangawanda open market have been neglected, abandoned or left incomplete when new administrations take Office.

**DEEPLY CONCERNED THAT**, the deliberate or negligent abandonment of these projects results in massive losses of public funds, denial of essential services, duplication of development plans and direct violation of the principles of continuity of government and the rights of the people to development.

**NOTING THAT**, these projects were initiated through public participation, funded using public resources and were intended to improve livelihoods, enhance access to water, improve mobility and safety and boost local trade and economic activities.

**FURTHER NOTING THAT**, public projects are public assets not political assets and therefore should be protected from political interference, regime changes or personal interests.

**THIS ASSEMBLY RESOLVES THAT:**

1. The County Executive Member for public works and infrastructure together with the County Executive Member for Finance shall submit to this Assembly within 30 days a full report detailing. The current status of the Mai Mekoni Water Project, the Myabogi Footbridge, the Mtangawanda Open Market and all other stalled or neglected County projects initiated since FY 2017/2018.
2. No ongoing funded or partially completed public project shall be abandoned by any incoming regime without written justification

**Deputy Speaker** (MCA Paul Kimani Njuguna): Next Order

**Clerk-at-the-Table:** Statements

### STATEMENTS

**Deputy Speaker** (MCA Paul Kimani Njuguna): I think Honorable Barisa Deko Bana is not in the House, so I defer this Statement to the next Sitting.

Next Order

**Clerk-at-the-Table:** Motion

### MOTION

*HOJA KUHUSU UZALISHAJI WA MBUZI DUME (BREEDING BUCKS) KATIKA  
KAUNTI YA LAMU*

**MCA Francis Ngure Gakonga** (*Bahari*): Asante Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika nimesimama kutoa hoja kuhusu uzalishaji wa mbuzi dume katika Kaunti ya Lamu.

**KWAMBA**, ufugaji ni mojawapo ya nguzo kuu za uchumi wa Kaunti ya Lamu, na wananchi wengi hasa katika maeneo ya mashambani hutegemea ufugaji wa mbuzi kama chanzo cha kipato na lishe.

**NA KWAMBA**, licha ya umuhimu huo, wakulima wengi wanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa mbuzi dume wa ubora wa juu kwa ajili ya kuzalisha mbuzi bora, jambo linalochangia kudumaa kwa uzalishaji na kupungua kwa kipato cha wafugaji.

**NA KWAMBA**, uwepo wa mpango wa Kaunti wa kuzalisha na kusambaza mbuzi dume wa kisasa kwa wakulima utasaidia kuboresha ubora wa uzao, kuongeza uzalishaji wa nyama na maziwa na kuinua kipato cha wakulima.

**SASA HIVYO BASI**, Bunge hili la Kaunti linaazimia kwamba:-

1. Serikali ya Kaunti ya Lamu, kupitia Idara ya kilimo, mifugo na uvuvi ianzishe mpango maalum wa uzalishaji wa mbuzi dume wa kisasa katika vituo vya mifugo vilivyopo Kaunti hii.
2. Serikali ihakikishe kwamba mbuzi hao dume wanazalishwa kutoka kwa aina bora za mbuzi wanaofaa kwa mazingira ya Lamu kama vile Galla, Somali na Alpine.
3. Idara husika iweke utaratibu wa usambazaji wa mbuzi dume hao kwa vikundi vya wafugaji na vituo vya uzalishaji vijijini kwa bei nafuu au kwa mpango wa mkono.
4. Serikali ya Kaunti itenge fedha maalum katika bajeti ya mwaka ujao kwa utekelezaji wa mpango huu, ikiwemo gharama za malisho, chanjo na utafiti wa kijenetiki.

Bwana Naibu Spika ninaomba nieleze hoja hii kwa kina, kusema kweli Kaunti yetu ya Lamu inategemea ufugaji wa ng'ombe zaidi kwa ajili ya kupata nyama na maziwa. Na kwa sababu hiyo Bwana Naibu Spika ufugaji wa mbuzi umerudi chini kabisa ndiposa nilikaa chini na kufikiria ya kwamba kuna vitamini A ambayo inapatikana kwa kiwango kikubwa kwa maziwa ya mbuzi pekee. Na kwa sababu hiyo unapokwenda kununua nyama katika buchari zilizoko vijijini utapata ya kwamba kuna upungufu mkubwa wa nyama ya mbuzi kupatikana ukilinganisha na nyama ya kondoo na nyama ya ng'ombe.

Bwana Naibu Spika kuna mbuzi aina tatu ambao wametajwa katika hoja hii wakiwemo Gala ambaye hutoa nyama nyingi sana, kuna Alpine ambaye hutoa maziwa mingi sana na mwisho ni mbuzi aina ya Boran ambaye pia hutoa nyama nyingi sana. Bwana Naibu Spika ninaamini katika Kaunti yetu ya Lamu kuna vikundi vingi ambavyo vimeundwa na wakati kunatokea miradi basi wananchi wanapata fursa ya kwenda kufundishwa namna ya kujikuza kiuchumi. Kwa hivyo ni vizuri Kaunti yetu ya Lamu iweze kutenga bajeti ya kuweza kuyasaidia makundi

haya kupata mbuzi ambao wataendana na hali ya hewa ilioko katika Kaunti hii yetu ya Lamu ili waweze kukua vizuri.

Bwana Naibu Spika tuko na vituo vingi na ni vizuri idara husika ya maswala ya ufugaji iweze kuzunguka Wadi zote 10 na kufanya utafiti na waone ya kwamba mbuzi hao wanastahili kukaa sehemu gani ili zao la maziwa liweze kuongezeka maradufu.

Bwana Naibu Spika, maziwa ya mbuzi yana chembe ndogo ya mafuta na zina urahisi wa kumenyeka ikilinganishwa na maziwa ya ng'ombe. Pia utapata ya kwamba maziwa ya mbuzi yana protini nyepesi ikilinganishwa na maziwa ya ng'ombe ambayo yako na protini ya juu zaidi. Kwa hivyo hoja hii imekuja kwa wakati mwafaka kwa sababu kuna uhaba wa nyama ya mbuzi katika Kaunti yetu ya Lamu.

### *Seconder*

**MCA Hope Wanjiku Mwaura (Nominated):** Thank you Mr Deputy Speaker for giving me this opportunity. Mr Deputy Speaker I stand to support and second this motion that has been brought forward by Honorable Gakonga. This motion is not only about goat, its a motion that bring dignity and economic empowerment to the people of Lamu County. When they will be improved goats breed in our County it will transform to an increase in economy in the County. It will also help reduce the rate of unemployment because our youths in our County will engage in farming.

Mr Deputy Speaker, we all know that most of the improved breeds are normally expensive and our farmers cannot afford good breeds. So when the County Government comes into this motion, the farmers will be at advantageous position. We also know that there are some Counties in our Country that have implemented this program for example Nyeri and Laikipia. So when this motion will be passed and adopted by the County Government the market prices of our goats will go higher, therefore our farmers will be able to sustain their livelihoods better.

## Motion Proposed

**Members Contributions**

**MCA Aisha Ali Abdurahman** (*Nominated*): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Gakonga ukizingatia ya kwamba nimetoka katika jamii ya wafugaji. Bwana Naibu Spika Kaunti yetu ina sehemu nzuri za malisho ya mifugo na miradi ya World Bank ikitufikia tunasambaziwa mifugo. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba tunapewa ng'ombe peke yake, kwa hivyo ni muhimu sisi kama Waheshimiwa tutilie mkazo jambo hili ili tuweze kuongezewa mbuzi kwa sababu wana maziwa ya kutosha kushinda ng'ombe.

**MCA Shekhuna Abbas Shekhuna** (*Mkomani*): Asante sana Bwana Naibu Spika, kwanza ningependa kumpongeza Mheshimiwa Gakonga kwa kuleta hoja kama hii. Bwana Naibu Spika Kaunti yetu iko na rutba ya kulisha mifugo ambapo Kaunti jirani wanalisha mifugo yao katika ardhi zetu. Na nina imani hoja hii ikipita basi Kaunti yetu itaweza kusonga mbele kiuchumi.

**MCA John Mburu Gitonga** (*Hongwe*): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Gakonga. Na kusema kweli tukipata mbegu zinazostahili kilimo kitaweza kunawiri na mifugo itaweza kutowa maziwa na nyama za kutosha.

**MCA James Njaaga Kariuki** (*Hindi*): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika kama Waheshimiwa wenzangu walivyochangia hoja hii utakuta ya kwamba katika Kaunti yetu ya Lamu tuna mandhari nzuri sana ya ukulima na ufugaji. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba tunatumia mbinu ya zamani ambayo haina mapato mazuri. Kwa hivyo sisi kama Waheshimiwa tunafaa kuwaelimisha wananchi na kuwatafutia mbegu ambazo zitaweza kuwabadilisha hawa wanyama wetu. Kwa hivyo hata tukiletewa dume kwa njia ya mkopo hatimaye tutaweza kulipa polepole na kukamilisha deni hilo.

Kwa hivyo ni wakati mwafaka kwa Kaunti yetu ya Lamu kupitia Idara ya kilimo, uvuvi na ufugaji waweze kuweka mikakati kabambe ya kuweza kuwashika vizuri hawa wakulima na tuweze kusonga mbele kiuchumi na kimaendeleo.

**MCA Beatrice Wamaitha Munge** (*Nominated*): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii, pili ningependa kumpongeza mtoa hoja Mheshimiwa Gakonga. Bwana Naibu Spika mbuzi ana maziwa yenye rutba muhimu sana kushinda maziwa ya ng'ombe na hata nyama yake ni nyororo. Pia tutaweza kupata mbolea katika mashamba yetu kupitia mbuzi hawa bora. Mbuzi hawa bora wanaweza kustahamili hali yoyote ya anga, kwa hayo machache namalizia kwa kuunga.

#### **Mover's Response**

**MCA Francis Ngure Gakonga** (*Bahari*): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika ningependa kuwapongeza Waheshimiwa waliochangia hoja hii kwa sababu nimeona wana haja kubwa ya kuona hoja hii ipite ili tuweze kuwasaidia wafugaji wetu. Hoja hii nimeweza kuileta kwa sababu wale wafugaji tulionao hawana mafunzo bora kuhusu ufugaji. Bwana Naibu Spika nimemsikia Mheshimiwa Hope akitaja Kaunti ya Nyeri na Laikipia ambazo zina mipango kama hii zetu lakini kusema kweli bado kuna Kaunti nyingi ambazo zina mipango haya kama vile Kwale, Kirinyanga na Busia. Pia Mheshimiwa Beatrice ameongezea kwa kusema ya kwamba kinyesi cha mifugo hao kitakuwa ni mbolea katika mashamba yetu. Bwana Naibu Spika inasikitisha kuona ya kwamba kila mwaka tunatenga bajeti ya kusaidia wakulima wa pamba, nazi na korosho lakini hatutengi bajeti ya ufugaji.

**Deputy Speaker** (MCA Paul Kimani Njuguna): Asanteni sana Waheshimiwa, pia ningependa kumsisitiza Katibu wa Bunge azidi kutengeneza hoja za kiswahili ukizingatia ya kwamba kiswahili kimenoga katika Kaunti yetu ya Lamu. Na wananchi wangependa kufahamu yanayojiri katika Bunge letu la Lamu.

(Question put and agreed upon)

**Deputy Speaker** (MCA Paul Kimani Njuguna): Honorable Members, there being no other business, the Assembly stands adjourned tomorrow Wednesday 10<sup>th</sup> December 2025 at 10:30am.

*The Assembly rose at 4:30p.m.*